


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



Tarehe 21/10/2021

**TANGAZO**

ZABUNI YA MAFUNDI KUJENGA WODI YA WANAWAKE KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA SIHA.

1. Halmashauri ya Wilaya ya Siha imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya Wanawake katika hospitali ya Wilaya Siha kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha anawaalika mafundi wenye sifa na uzoefu wa kutosha kuleta gharama zao za ufundi kama ilivyobainishwa kwenye jedwali hapa chini

NAMBA YA ZABUNI	JINA LA ZABUNI
LGA/SDC/050/2021/W/05	Ujenzi wa Wodi ya wanawake

3. Masharti kwa waombaji ni:
  - i. Fundi awe na ujuzi wa kujenga majengo ya Serikali nauwezo wa kusoma na kutafsiri ramani
  - ii. Fundi awasilishe uthibitisho wa uzoefu wa kazi za serikali alizozifanya kwa angalau mbili na kupatiwa certificate ya malipo ya mwisho.
  - iii. Fundi awe na anwani ya makazi inayoeleweka pamoja na akaunti namba ya Benki
  - iv. Fundi atalazimika kuomba kazi husika kwa barua itakayopitishwa na Mtendaji wa Kijiji anapoishi na ibandikwe picha yake (pass port size)
  - v. Waombaji wanatakiwa kutembelea eneo la kazi kabla ya kuwasilisha maombi na kupata maelekezo ya kazi husika ikiwemo vipimo na ramani ya ujenzi kwenye ofisi ya Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya Siha.
  - vi. Waombaji watakaowasilisha vyeti vya ufundi watafikiriwa zaidi.
  - vii. Waombaji watapata fomu za kujaza zenye maelekezo ya kazi inayotakiwa kufanyika, fomu hizo zinapatikana ofisi ya manunuzi na ugavi katika Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Siha.

- viii. Nukuu ya bei zikiwa zimejazwa vizuri na kufungwa katika bahasha yenye lakiri juu ya bahasha zikiwa zimeandikwa "MAOMBI YA KUJENGA WODI YA WANAWAKE KATIKA HOSPITALI YA WILAYA SIHA

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Siha  
S.L.P 129  
SANYA JUU,  
SIHA

Maombi yawasilishwe ghorofa ya kwanza Ofisi ya Manunuzi na Ugavi, Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Siha.

- ix. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 28/10/2021 saa 4:00 asubuhi siku ya Jumatatu.
- x. Maombi yatakayochelewa, ambayo hayatapokelewa na ambayo hayakufunguliwa wakati wa ufunguzi hayatapokelewa na hayatashughulikiwa.

Limetolewa na:



Mangali D.E

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA SIHA

**MKURUGENZI MTENDAJI (w.)  
SIHA**